

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

*Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : press@ikulu.go.tz  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)*



*OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.*

*Dar es Salaam.  
27 Desemba, 2021.*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi wa viongozi wafuatao: -

1. Amemteua Jaji Jacob Casthom Mwambegele kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Jaji Mwambegele ni Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Jaji Mwambegele anachukua nafasi ya Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani Semistocles Kaijage ambaye amemaliza muda wake.
2. Amemteua Jaji Mwanaisha Athuman Kwariko kuwa Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Jaji Kwariko anachukua nafasi iliyaoachwa wazi na Jaji Jacob Casthom Mwambegele.
3. Amemteua Jaji Sam Mpaya Rumanyika, Jaji wa Mahakama Kuu kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.
4. Amemteua Prof. Khamis O. Dihenga kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB). Prof. Dihenga anahudumu kwa Mkataba katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Morogoro. Prof. Dihenga anachukua nafasi ya Prof. William A. L. Anangisye aliyemaliza muda wake.
5. Amemteua Dkt. Mussa Muhidin Kissaka, Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

Uteuzi huu umeanza tarehe 23 Desemba, 2021.

A blue ink signature of Jaffar Haniu.

Jaffar Haniu

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu.